



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**



Tarehe: 06/01/2022

**TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA
UKAMILISHAJI WA VYUMBA VYA MADARASA NA MAABARA**

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa na maabara.
2. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inakaribisha Mafundi wa kazi za Mikataba ya Muda Mfupi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za Ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kwa ajili ya Ujenzi kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account" katika fani zifuatazo:-
 - i. Fundi Uashi (ambao pia utajumuisha upakaji wa rangi na Ufundi umeme)
 - ii. Fundi Aluminium (Utengenezaji wa madirisha)
 - iii. Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).

Sifa za muombaji

- i. Awe Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii. Awe na Namba ya Utambulisho wa Ulipaji Kodi (TIN)
- iii. Awe na akaunti kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe
- iv. Awe na ujuzi wa kusoma ramani na kuelezea.
- v. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi za serikali na mwenye uelewa na taratibu zake. Aambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha uzoefu wake katika kufanya kazi za Serikali (yaani aambatanishe nakala za barua za tuzo za kazi alizowahi kufanya, nakala za mikataba ya kazi za ujenzi, nakala za Hati za Malipo za kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021).
- vi. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha (Mtaji) wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi pasipo kuomba kulipwa malipo ya awali (Advance Payments);

